BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Nane – Tarehe 20 Februari, 2026.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Itasomwa.

## MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

48. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

    Kwa muda mrefu kumeongezeka malalamiko ya wananchi wanaolima mpunga katika mabonde ya Kinoe kwa Pape na Tumbe kwa Chakasa kuingiliwa na maji chumvi katika mabonde yao. Wananchi hao huyakinga maji chumvi hayo kwa kujenga matuta ya kienyeji ambayo baada ya muda, huzidiwa na maji chumvi hayo kupita, kufika na kuleta athari katika mashamba yao.

    Pamoja na kuahidi kuliondoa tatizo hilo kwa muda mrefu sasa, je Seikali ina mpango gani wa kuzitekeleza ahadi zake kwa haraka.

### Wizara ya Fedha na Mipango:

205. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

    Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Nane imefanya vizuri katika jitihada zake za kuifungua Pemba kwa kuvutia wawekezaji. Uingizaji wa chakula kwa Pemba umekuwa nafuu

baada ya kupunguzwa kwa ushuru.

(a) Kwa nini mpango wa kupunguza ushuru kwa bidhaa za chakula usifanywe vilevile kwa bidhaa na huduma nyengine ili kuvutia zaidi wawekezaji kwa upande wa Pemba.

(b) Je, Serikali inao mpango wa kuweka vivutio maalumu kwa wawekezaji wakubwa na wadogo, ili kuzidi kuifungua Pemba na kutimiza azma ya Mheshimiwa Rais.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

5. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuuhakikisha usalama wa wanawake mahali pa kazi, ili kuzuia unyanyasaji na ubaguzi.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

189. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Mwakilishi Jimbo la Ole) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa tunavyo vyuo vingi vya kati na juu vinavyotoa programu ambazo sio za kipaumbele kwa sasa kwa Zanzibar na matokeo yake huzalisha wataalamu ambao hawahitajiki katika soko la ajira.

(a) Je, Serikali imewahi kufanya utafiti au tathmini ya programu zinazotolewa na vyuo na mlinganisho wake wa uajiri wa programu hizo katika soko la ajira.

(b) Kwa nini Serikali haiweki utaratibu wa kufanya utafiti kwa kushirikiana na vyuo kabla ya kuanzisha programu husika ili kujua programu za kipaumbele.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

52. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Mpango wa Serikali ya Awamu ya Nane kupitia maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni kuwajengea wananchi wa Zanzibar nyumba, ili

waweze kuishi katika makaazi bora nchi nzima.

Je, ni maeneo gani yatakayojengwa nyumba hizo kwa upande wa Pemba.

## Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

63. MHESHIMIWA JABU MAKAME JUMA (Nafas za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Lugha ya Kiswahili imetangazwa na Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kuwa ni lugha ya kazi, ikiwa ni lugha ya kwanza ya kiafrika kuwa na siku yake maalumu ya kuadhimishwa, huku nchi yetu ya Zanzibar ikipata bahati ya kuwa ni kitovu cha lugha hii.

(a) Ni lini ofisi za Baraza la Kiswahili zilizopo Zanzibar zitakuwa na hadhi inayoendana na hadhi ya lugha hii Barani Afrika na duniani kote.

(b) Ni vijana wangapi wa Kizanzibari wamenufaika na fursa za Kiswahili nje ya nchi tangu kutangazwa kuwa Kiswahili ni lugha ya kazi katika taasisi za kimataifa.

## Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:

139. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Mabaharia wazawa walio wengi wanakimbilia kufanya kazi nje ya nchi kwa kufuata mishahara mikubwa, inayoendana na mfumo wa mishahara ya Shirika la Kimataifa la Usafiri Baharini (IMO), ukilinganisha na wanayolipwa hapa nchini.

Je, lini Serikali italiingilia kati jambo hili ili mabaharia wa Zanzibar na waofanya kazi ndani ya Zanzibar, wafaidike kwenye mfumo wa mishahara wa IMO.

179. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kwa muda mrefu sasa, wananchi wa jimbo la Uzini, shehia ya Koani, eneo la Kibonde Maji, wanapata usumbufu mkubwa unaosababishwa na ubovu wa barabara ya Koani Kibonde Maji.

(a) Ni lini Serikali itaifanyia matengenezo na kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

(b) Ni lini Mheshimiwa Waziri utafanya ziara katika barabara hiyo, ili wananchi wapate kusikia kauli yako juu ya ujenzi wa barabara hiyo.

(c) Kwa kuwa barabara hiyo huzidi kuharibika katika kipindi cha mvua za masika, je Serikali inatoa kauli gani kwa watumiaji wa barabara hiyo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

125. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMED (Jimbo la Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali ya Awamu ya Nane imeweka dhamira ya kuimarisha uzalishaji wa bidhaa hasa za kilimo na mifugo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wakulima na wafugaji kutumia mbinu mpya za kisasa (za kutumia teknolojia ya kilimo na ufugaji) na kuachana na kutumia mbinu za asili.

**Wizara ya Afya:**

39. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Moja ya malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kutoa huduma za afya bure kwa wananchi wote na kuimarisha huduma za afya katika vituo vya Serikali, ili kuwaondoshea usumbufu na kupata huduma zisizoridhisha wananchi wake na kuwawezesha kupata huduma nzuri, haraka na salama.

(a) Ni lini Serikali itawasaidia wananchi na kina mama wajawazito wanaotumia Kituo cha Afya cha Ukutini Pemba, kuweza kupata kipimo cha ULTRASOUND.

(b) Ni upi mpango wa Serikali wa kutatua changamoto za usafiri wa gari ya kubebea wagonjwa (AMBULANCE) katika vituo vya kujifungulia kina mama vya Pujini na Wambaa.

(c) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya ujenzi wa nyumba za daktari kwenye Vituo vya Afya Pujini, Ukutini na Wambaa.

215. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na malalamiko kwa wafanyakazi wa hospitali kuhusu kuchelewa kwa malipo ya fedha za bima ambazo zinaingia Serikalini moja kwa moja na hospitali inapata fedha hizo kupitia fedha za matumizi mengineyo (O/C) ambazo zinachelewa.

(a) Kwa nini fedha za bima zisiwekewe mgao kwa asilimia maalumu baina ya Serikali na hosptali ili wafanyakazi walipwe mapema badala ya kusubiri (O/C).

(b) Kwa kuwa baadhi ya hospitali kubwa Tanzania bara zinaweka utaratibu huo wa malipo, kuna ugumu gani kuwa na mfumo kama huo ulioelezwa katika swali (a).

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

70. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Ni kwa nini huduma ya maji katika vijiji vingi vya shehia ya Mgogoni imekuwa ni changamoto.

**Zanzibar,**
**20 Februari, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**